CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

MOROGORO

NAFASI ZA KAZI

Limetolewa tarehe 22.08.2017

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kinakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi mbalimbali za kazi.Waombaji wawasilishe barua iliyoandikwa kwa mkono, ikiwa na Maelezo binafsi ya mwombaji (CV), nakala ya Cheti cha Kuzaliwa, Vyeti vya Taaluma na Ujuzi (Kama vipo) pamoja na majina mawili ya wadhamini pamoja na anuani zao, barua pepe na namba za simu na kisha maombi hayo yatumwe kwenye anuani hii; **NAIBU MAKAMU WA MKUU WA CHUO (UTAWALA NA FEDHA), S.L.P 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO;** imfikie ndani ya **WIKI MBILI** tangu tarehe ya tangazo hili.

1. NAFASI: WAHUDUMU WA MILIKI III – (ESTATES ATTENDANT III) (nafasi - 23) – Kampasi Kuu SUA - Morogoro, Kampasi ya Olmotonyi– Arusha na Kampasi ya Mazumbai – Lushoto.

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha maeneo yote yanayozunguka Chuo
- Kusafisha vichaka na kufyeka majani katika maeneo ya Chuo.
- Kukusanya na kuchoma takataka zote zinazozunguka maeneo ya Chuo.
- Kulinda na kutunza miundo mbinu ya Chuo ili kusaidia kuepukana na majanga mbalimbali kama vile moto.
- Kutunza uoto uliopo katika maeneo yanayozunguka Chuo.
- Kushughulikia bustani na maua katika maeneo ya Chuo.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

2. NAFASI: MHUDUMU WA SHAMBA/MIFUGO III(FIELD ATTENDANT III) (Nafasi-80) – Kampasi Kuu SUA - Morogoro, Kampasi ya Olmotonyi – Arusha na Kampasi ya Mazumbai – Lushoto.

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusimamia na kutunza mazingira yanayozunguka Mashamba Darasa ya Chuo, Vitalu vya Mimea Vipando, Bustani na Kitengo cha Uzalishaji wa miche ya MbogaMboga na Matunda.
- Kutunza na Kuwalisha Wanyama wote wanaofugwa katika Shamba Darasa la Mifugo la Chuo.
- Kutunza na kumwagilia vitalu vya maonesho vilivyopo katika maeneo ya maonesho mbalimbali yanayosimamiwa/yanayomilikiwana Chuo.
- Kuhakikisha usalama katika Shamba Darasa la Chuo, Hifadhi ya Mimea Vipando, Bustani na Kitengo cha Uzalishaji wa miche ya MbogaMboga na Matunda ili kuyaepusha na mazingira hatarishi yanayoweza kusababisha uharibifu kama vile moto.
- Kufanya kazi zinazohusiana na Ukamuaji wa maziwa kwa ng'ombe na Mbuzi, Uandaaji na Utunzaji wa Malisho na kusimamia Kitengo cha Kuku pamoja na kazi nyingine zinazoendana na hizo chini ya usimamizi wa "Field Assistants/Officers.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

3. NAFASI: MHUDUMU WA MADARASA/MABWENI III (HALLS ATTENDANT III) (Nafasi -2) –Kampasi Kuu SUA - Morogoro

SIFA ZINAZOHITAJIKA:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha mazingira yanayozunguka madarasa, kumbi mbalimbali za Chuo na maeneo ya malazi ya wanafunzi.
- Kutunza kumbi mbalimbali za Chuo na Madarasa na kutoa taarifa pale inapotokea tatizo lolote la uharibifu.
- Kusafisha vyoo vilivyopo kwenye kumbi mbalimbali za Chuo na Madarasa kwa kadri itakavyohitajka.
- Kuhakikisha Usalama, kutunza na kulinda mali za Chuo zinazotumika kwenye kumbi, vyumba vya Mihadhara na Madarasa Chuo.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni
UMRI: Umri usiozidi miaka 45
MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

4. NAFASI: MHUDUMU WA MAABARA III (LABORATORY ATTENDANT III) (Nafasi-15) –Kampasi Kuu SUA - Morogoro

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwenye Cheti cha ufaulu cha kidato cha nne. Kwa waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo au wenye mafunzo ya awali ya masuala ya maabara watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha mazingira yote yanayozunguka maabara za Chuo
- Kutunza maabara zote za Chuo na kutoa taarifa kwa Msimamizi wa Maabara endapo kutatokea tatizo lolote.
- Kuhakikisha usalama wa maabara zote za Chuo.
- Kusafisha vifaa vya maabara chini ya uangalizi wa Msimamizi wa Maabara.
- Kubeba vitendanishi na vifaa mbalimbali vya maabara na kuvipeleka panapostahili chini ya uangalizi na usimamizi wa “Laboratory Assistant/Technician”.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

5. NAFASI: MHUDUMU WA OFISI III (OFFICE ATTENDANT III) (Nafasi-1) – Kitengo cha Ugavi na Manunuzi cha SUA – Ofisi ya Dar-es-Salaam

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha Mazingira yanayozunguka Ofisi
- Kushiriki maandalizi ya Vikao mbalimbali.
- Kufanya usafi wa ndani na nje ya Ofisi.
- Kuhakikisha vifaa vya ofisi vinahifadhiwa vizuri na kutunzwa ipasavyo
- Kupokea na Kusambaza barua, majalada pamoja na nyaraka nyingine za kiofisi.
- Kuandaa Kumbi za Vikao na Kutoa huduma mbalimbali wakati wa vikao
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

6. NAFASI: MHUDUMU WA MISITU III (FOREST ATTENDANT III) (Nafasi -7) - Kampasi ya Olmotonyi – Arusha

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha mazingira yanayozunguka misitu.

- Kuhakikisha usalama katika hifadhi ya misitu ili kuepukana na matukio kama vile ya moto, wizi, uvamizi wa misitu na uharibifu wa aina nyingine.
- Kuhakikisha Misitu inatunzwa ipasavyo.
- Kusaidia kuanda vitalu vya misitu kwa ajili ya darasa kwa wanafunzi na upandwaji.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

7. NAFASI: MHUDUMU WA MAZAO YA MISITU III (LOGGER ATTENDANT III) (Nafasi-4) – Kampasi ya Olmotonyi – Arusha.

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kusafisha karakana, mashine za kuchana/kukata magogo na vifaa mbalimbali.
- Kuwezesha usafirishaji wa magogo kutoka msituni hadi kwenye mitambo/mashine za kuchana/kukata magogo; pia kutoka sehemu hadi nyingine katika maeneo ya Karakana.
- Kumsaidia Mpasuaji na Mkataji wa magogo katika zoezi la kuchana magogo.
- Kusaidia utunzaji wa magogo nambao katika eneo la uandaaji magogo hayo.
- Kuhakikisha usalama wa mitambo pamoja na mashine zinazotumika katika shughuli hizo ilikuzuia majanga kama ya moto.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina

8. NAFASI: MHUDUMU WA KARAKANA III (WORKSHOP ATTENDANT III) (Nafasi-9)-Kampasi Kuu SUA – Morogoro na Kampasi ya Olmotonyi – Arusha

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye Cheti cha ufaulu wa kidato cha nne (Form IV). Waombaji waliowahi kufanyakazi kwenye mazingira yanayofanana na kazi hiyo watapewa kipaumbele.

MAJUKUMU YA KAZI:

- Kufanya usafi katika karakana zote za Chuo na Mitambo na kufanyia usafi vifaa vilivyopo.
- Kusafisha mazingira yote yanayozunguka Karakana za Chuo.
- Kutunza na kuhifadhi vifaa vyote vilivyopo katika karakana
- Kusaidia watafiti, walimu na mafundi mchundo pale panapohitajika wakati wa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi yakiendelea.
- Kuhamisha mitambo, vifaa na malighafi zote zitokanazo na karakana (pale inapohitajika).
- Kuhakikisha usalama wa mazingira ya Karakana na kutoa taarifa za hitilafu au uharibifu wowote wa vifaa vya Karakana kwa Msimamizi wa Karakana.
- Kutekeleza majukumu mengine yanayoendana na kazi hiyo kama atakavyopangiwa na Msimamizi wa Kazi.

MASHARTI YA AJIRA: Mkataba wa Kudumu na Malipo ya Uzeeni

UMRI: Umri usiozidi miaka 45

MSHAHARA: Kwa mujibu wa Nyaraka za Mishahara za Msajili wa Hazina